JARIDA LA USHIRIKA

ISSN 2714 - 2175 Toleo Na. 17 Januari - Machi, 2025

MAFANIKIO YA SEKTA YA USHIRIKA KATIKA MIAKA MINNE (2021/22 – 2024/25) YA SERIKALI YA AWAMU YA SITA











Ushirika - Pamoja Tujenge Uchumi

YALIYOMO

1. KUTOKA KWA MRAJIS.....1

2. MAFANIKIO YA SEKTA YA USHIRIKA KATIKA KIPINDI CHA MIAKA MINNE YA SERIKALI YA AWAMU YA TANO.....2

3. WANAUSHIRIKA ZANZIBAR WAFANYA ZIARA KATIKA VYAMA VYA USHIRIKA MKOANI DODOMA.....8

4. BENKI YA USHIRIKA YATAKIWA KUTUMIA FURSA ZA USHIRIKA KUJIENDESHA KIBIASHARA.....10

5. RAIS DKT. SAMIA AWATAKA WANAWAKE KUWEKEZA KATIKA MALEZI.....12

6. MAFUNZO YA USIMAMIZI WA VYAMA VYA USHIRIKA KWA MAAFISA USHIRIKA YANAVYOONGEZA TIJA KATIKA USHIRIKA.....15

7. AFRIKA INAHITAJI KUREJESHA HADHI YAKE KWENYE TASNIA YA KAHAWA DUNIANI - RAIS DKT. SAMIA.....19

8. SERIKALI YAJIDHATITI KUBORESHA SEKTA YA KILIMO – DKT BITEKO.....20

9. CHAMA KIKUU CHA USHIRIKA NYANZA CHAZINDUA UVUNAJI WA SAMAKI WA VIZIMBA.....21

10. UNION NA SACCOS KUBWA ZATAKIWA KUAJIRI WAKAGUZI WA NDANI.....22

11. TENGENEZENI MIFUMO,TARATIBU NA KANUNI IMARA ILI KUENDELEZA VYAMA - NAIBU KATIBU MKUU KILIMO.....24

12. TCDC NA WAKANDI ZASAINI 'MoU' KUVIIMARISHA VYAMA VYA USHIRIKA KIDIGITALI.....25

13. NANYUMBU AMCOS YANUNUA GARI LENYE THAMANI YA SHILINGI MIL.185.....26

Kutoka kwa Mrajis



Dkt. Benson O. Ndiege
Mrajis na Mtendaji Mkuu wa TCDC

Ni wasaa mwingine Tume ya Maendeleo ya Ushirika (TCDC) inakuletea Jarida Toleo Na.17 lenye habari, matukio pamoja na makala za elimu ya Ushirika ili kuhabarisha na kuonesha fursa zilizopo katika Sekta ya Ushirika katika Kipindi cha Miaka minne ya Uongozi wa serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Katika Kipindi cha uongozi wa serikali ya awamu ya sita Sekta ya Ushirika imeendelea kuimarika kwa usimamizi wa vyama ambapo hati safi zimongezeka kutoka vyama 339 mwaka 2021/22 hadi kufikia vyama 631 Mwaka 2023/24.

Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo (SACCOS) vimeendelea kuwahudumia wanachama wake kwa kutoa huduma za akiba, amana na mikopo, hadi kufikia mwaka 2024/2025, Akiba na Mikopo katika SACCOS imeongezeka kutoka Shilingi Bilioni 576.0 mwaka 2021/2022 kufikia Shilingi Bilioni 966.9 mwaka 2023/2024.

Aidha, masoko ya mazao yameongezeka kupitia Mifumo rasmi ya Ushirika kutokana na bei za mazao kupanda hadi kufikia Februari, 2025, jumla ya tani 2,225,397.56 zenye thamani ya Shilingi Trilioni 4.2 zilikusanywa na kuuzwa kupitia mfumo rasmi wa Ushirika ukilinganisha na Tani 591,268.122.

Vyama vya Ushirika vimekuwa ni njia ya uhakika ya kufikisha Pembejeo kwa Wakulima ambapo thamani ya pembejeo za kilimo zilizonunuliwa na kusambazwa kupitia vyama vya vya Ushirika imeongezeka kufikia Shilingi 847,043,539,044, msimu wa 2024/25 ikilinganishwa na pembejeo zenye thamani ya Shilingi 9,010,403,964.00 kwa mwaka 2021/2022.

Viwanda vinavyomilikiwa na Vyama vya Ushirika Hadi kufikia mwaka 2024/25 jumla ya viwanda vinamilikiwa na Vyama vya Ushirika vimefikia 331 ukilinganisha na viwanada 267 mwaka 2021/2022. Viwanda hivyo vimesaidia kuongeza thamani ya mazao ya wakulima na kuongeza bei ya mazao hayo sokoni

Ili Sekta ya Ushirika iendelee kukua na kuongeza Tija ya Uchumi Tume itaendelea kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia vipaumbele vyake ikiwemo kuwezesha Uwekezaji katika mifumo ya kisasa ya kidijitali katika Vyama vya Ushirika.

katika kuimarisha sekta ya Ushirika Serikali inatekeleza vipaumele vifuatavyo; Uwekezaji katika mifumo ya kisasa ya kidigitali; kuimarisha benki ya ushirika nchini; kuhamasisha mfumo wa ushirika kujiendesha kibiashara; kuboresha sera,sheria na Usimamizi wa Ushirika.

Aidha, vipaumbele vingine ni pamoja na kuhamasisha Ushirika kwenye sekta mbalimbali na makundi maalumu; kuimarisha uwekezaji wa mali za ushirika katika uzalishaji; kushirikiana na wadau mbalimbali katika kutatua changamoto zilizopo kwenye ushirika; na kuboresha maslahi ya watumishi.

Ushirika - Pamoja Tujenge Uchumi



MAFANIKIO YA SEKTA YA USHIRIKA KATIKA KIPINDI CHA MIAKA MINNE YA SERIKALI YA AWAMU YA SITA

Katika kipindi cha miaka minne (2021/22 - 2024/25) chini ya Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa, Dkt. Samia Suluhu Hassan, Sekta ya Ushirika imepata mafanikio yafuatayo:

1.1. Kuimarika kwa utendaji wa vyama vya Ushirika

Kutokana na kuimarishwa kwa usimamizi, Vyama vya Ushirika vimeendelea kuimarika katika utekelezaji wa shughuli zake kama ilivyobainishwa na Shirika la Ukaguzi wa Vyama vya Ushirika (COASCO).

Vyama vya Ushirika vilivyopata Hati safi vimeongezeka kutoka vyama 339 mwaka 2021/22 hadi kufikia vyama 631 Mwaka 2023/24. Aidha, Vyama vilivyopata Hati isiyoridhisha na maoni vimepungua kutoka Vyama 1,198 mwaka 2021/22 hadi vyama 263 mwaka 2023/24 na Hati mbaya zimepungua kutoka vyama 2,075 mwaka 2021/22 hadi 995 mwaka 2023/2024.

Hali hii inaashiria kuwa utendaji wa vyama vya ushirika umeimarika.

1.2. Kuimarika kwa Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo (SACCOS)

Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo (SACCOS) vimeendelea kuwahudumia wanachama wake kwa kutoa huduma mbalimbali kama vile Akiba, Amana na mikopo.

Hadi kufikia mwaka 2024/2025, Akiba na Mikopo katika SACCOS imeongezeka kutoka **Shilingi Bilioni 576.0** mwaka 2021/2022 kufikia **Shilingi Bilioni 966.9** mwaka 2023/2024, na Mikopo iliyotolewa kwa wanachama wa SACCOS imeongezeka kutoka **Shilingi Bilioni 798.0** mwaka 2021/2022 kufikia **Shilingi Trilioni 1.1 mwaka 2023/2024.**



Jengo linalomilikiwa na Bandarini SACCOS LTD ambapo ni Makao Makuu ya Chama hicho

1.3. Kuimarika kwa Matumizi ya Mifumo rasmi ya Masoko ya Mazao ya Wakulima

Wakulima wameendelea kukusanya na kuuza mazao yao kupitia mifumo rasmi ya masoko inayotumika katika Vyama vya Ushirika. Kuongezeka kwa mauzo kupitia Mifumo rasmi ya Ushirika kumesababisha mazao yanayouzwa kuongezeka na bei za mazao kupanda.

Hadi kufikia Februari, 2025, jumla ya **tani 2,225,397.56** zenye thamani ya **Shilingi Trilioni 4.2** zilikusanywa na kuuzwa kupitia mfumo rasmi wa Ushirika ukilinganisha na **Tani 591,268.122** zilizouzwa kwa thamani ya **Shilingi Trilioni 1.1** mwaka 2021/2022.

Aidha, ushuru uliokusanywa na Halmashauri umeongezeka kutoka **Shilingi Bilioni 33.7** mwaka 2021/2022 kufikia Shilingi Bilioni 64.1 mwaka 2023/2024

1.3.1. Kuimarika kwa Mauzo ya Moja kwa Moja ya mazao (Direct Sales):

Katika mwaka 2024/25 hadi kufikia Ushirika 1,084 viliuza Kahawa na Tumbaku moja kwa moja nje ya nchi (Direct Export) kiasi cha **Kilo 133,636,327.00** kwa thamani ya Dola za Kimarekani **344,811,215.00.**

Aidha katika mwaka 2023/24 Kiasi cha **Kilo 135,964,721.00** zenye thamani ya Dola za Kimarekani **325,562,067.32**

1.4. Kuongezeka kwa Upatikanaji na Usambazaji wa pembejeo za kilimo kupitia Vyama vya Ushirika.

Thamani ya pembejeo za kilimo zilizonunuliwa na kusambazwa kupitia Vyama vya Ushirika imeongezeka kufikia **Shilingi 847,043,539,044** msimu wa 2024/25 ikilinganishwa na pembejeo zenye thamani ya **Shilingi 9,010,403,964.00** kwa mwaka 2021/2022. Pembejeo zilizonunuliwa na kusambazwa kwa wakulima ni mbolea, viuatilifu (madawa), vifungashio, mbegu na miche kwa ajili ya mazao ya kahawa, pamba, korosho, Tumbaku, ufuta, alizeti, Mahindi na mpunga.

JE, WAJUA MAJUKUMU YA WAJUMBE WA BODI ZA VYAMA VYA USHIRIKA?

a) Kuandaa taratibu sahihi za fedha na kanuni muhimu kwa ajili ya kutunza kumbukumbu za shughuli za chama cha ushirika kwa uwazi na usahihi;

(b) Kuhakikisha kwamba hesabu za chama cha ushirika zimeandaliwa na kukaguliwa kwa mujibu wa matakwa ya Sheria, Kanuni na masharti ya chama;

(c) Kuwasilisha katika mkutano mkuu wa mwaka taarifa ya fedha iliyokaguliwa na taarifa ya Wakaguzi kwa Uongozi;

(d) Kuandaa makisio ya mapato na matumizi ya mwaka kabla ya kuyawasilisha katika mkutano mkuu;

(e) Kuwezesha ukaguzi wa vitabu vya hesabu kwa mtu yeyote aliyepewa mamlaka kuvikagua;

(g) Kuhakikisha kwamba masharti ya chama au mikataba inayowafunga kisheria wanachama kuhusiana na chama cha ushirika vinazingatiwa;

(h) Kuandaa mikataba, muundo na kanuni za utumishi za waajiriwa wa chama cha ushirika;

(i) Kutafuta na kupanga ajira za Meneja na watendaji wengine wakuu wa chama cha ushirika kwa misingi ya uhuishwaji wa mikataba ya kudumu;



Uzinduzi wa kiwanda cha kubangua Korosho uliofanywa na Waziri wa Kilimo, Mhe. Hussein Bashe, Oktoba 2024, kiwanda kinamilikiwa na Chama Kikuu cha Ushirika TANECU LTD, Mtwara



Kiwanda cha Kubangua Korosho cha TANECU LTD

1.5. Ongezeko la viwanda vinavyomilikiwa na Vyama vya Ushirika

Hadi kufikia mwaka 2024/25 jumla ya viwanda vinamilikiwa na Vyama vya Ushirika vimefikia **331** ukilinganisha na viwanada **267** mwaka 2021/2022.

Shughuli zinazofanywa na viwanda hivi ni uchambuaji wa pamba, ukoboaji wa mpunga, kahawa na mahindi, usindikaji wa maziwa, ukamuaji wa mafuta ya pamba, alizeti, karanga na ufuta, na ubanguaji wa korosho.



Wafanyakazi wa kiwanda cha kubangua Korosho cha Chama Kikuu cha Ushirika TANECU LTD, Mtwara

1.6. Kuongezeka kwa ajira katika Vyama vya Ushirika

Kuimarika kwa Vyama vya Ushirika kumefanikisha kuongezeka kwa wananchi walioajiriwa katika vyama hivyo kufikia **155,106** mwaka 2024/2025 ikilinganishwa na wananchi **100,100** waliopata ajira katika vyama mwaka 2020/21, ikiwa ni ongezeko la **asilimia 55.1**



Kiwanda cha Kubangua Kahawa cha WAMACU LTD - Mkoani Mara

1.7. Kuongezeka kwa matumizi ya TEHAMA katika uendeshaji wa shughuli za Ushirika na Matumizi ya mizani ya Kidigitali

1.7.1. Kuanzisha Mfumo wa Kidigitali wa Usimamizi wa Vyama

Katika kuimarisha usimamizi wa Vyama vya Ushirika kwa njia ya TEHAMA, Tume imeanzisha Mfumo wa usimamizi wa vyama vya Ushirika (MUVU) ambao umeunganishwa na Mifumo ya Taasisi tisa (9) ambayo ni Mfumo Mkuu Unganishi wa Serikali (GovESB), Mfumo wa Usimamizi wa Rasilimali (ERMS), Mfumo wa Ukusanyaji wa Malipo ya Serikali Kielektroniki (GePG),

Mfumo wa Wizara ya Kilimo (e-Kilimo), Mfumo wa Mizani ya kidigitali (Mkulima Hub), Mfumo wa Mfuko wa Bima ya Afya (NHIF), Mfumo wa Bodi ya Sukari (CANGROWERS-MIS), Mfumo wa ELCT ND SACCOS na Mfumo wa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA). Aidha, mpaka sasa Vyama 6,634 vimesajiliwa kwenye MUVU ambapo Vyama vya msingi ni **6,117,** Vyama vya Upili ni **75**, vyama vya Awali ni **441** na Shirikisho ni kimoja (**1**).

1.7.2. Kuimarika kwa matumizi ya Mizani za Kidigitali

Katika Kuimarisha matumizi ya Mizani za Kidigitali kwenye ununuzi wa mazao ya wakulima, hadi kufikia 2024/2025 jumla ya Mizani za Kidijitali 3,760 zenye thamani ya Shilingi Bilioni 13.3 ilinunuliwa na kusambazwa kwa Vyama vya Ushirika Vya Ushirika 992 ikilinganishwa na mwaka 2023/2024 ambapo Vyama vya ushirika vilikuwa na mizani za kidigitali 1,178.

Mizani hiyo inatumika na vyama vya Ushirika vinavyojishughulisha na mazao ya kahawa, korosho, ufuta, soya, mbaazi, kakao na tumbaku katika Mikoa ya Kagera, Lindi, Mbeya, Tabora, Mtwara, Ruvuma na Pwani.



Uzinduzi wa Mfumo wa kidigitali wa Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (MUVU) uliofanywa na Waziri wa Kilimo, Mhe. Hussein Bashe, Julai 2023



Mizani za kidigitali zilizonunuliwa na kutumika katika ununuzi wa mazao katika mikoa ya Kusini

1.8. Kuimarisha Uwekezaji wa mali za Ushirika katika uzalishaji

Katika mwaka 2024/25, Tume imeendelea kusimamia Vyama vya Ushirika kutambua na kuthaminisha mali za kudumu za Vyama ambazo zilikuwa zimechukuliwa na kutumika nje ya utaratibu. Hadi kufikia Februari 2025, jumla ya Vyama vya Ushirika 673 vimetambua, kuthaminisha na kuingiza mali 4,348 kwenye Mfumo wa MUVU, zenye thamani ya soko ya Shilingi 1,318,807,288,055.00

1.9. Kuanzishwa kwa Benki ya Taifa ya Ushirika

Benki ya Ushirika Tanzania ilianzishwa



Rais wa Jamhuri ya muungano wa Tanzania, Mh. Dkt. Samia Suluhu Hassan akikata Utepe kuashiria kuzinduliwa kwa Benki ya Ushirika Tanzania uliofanyika Jijini Dodoma.

kwa kuunganisha iliyokuwa Benki ya Ushirika Mkoa wa Kilimanjaro Ltd (KCBL) pamoja na Benki ya wananchi Tandahimba Ltd (TACOBA). Benki hii ilisajiliwa mnamo 26 Mei, 2024 na Mrajis wa Vyama vya Ushirika na kupewa Leseni ya uendeshaji wa biashara za mabenki kutoka kwa Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania mnamo

4 Oktoba 2024. Benki ya Ushirika imeanza na matawi matatu (3) (Tawi la Dodoma, Kilimanjaro na Tandahimba) na inamilikiwa na Vyama vya Ushirika kwa **asilimia 51** kama wawekezaji wakuu.

Uwekezaji wa hisa katika benki umeongezeka kutoka **Billion 15.7** 2022/2023 hadi kufikia **Billion 27.4** mwaka 2024/2025. Aidha, mtaji wa wana hisa umezidi kuimarika mpaka kufikia Shilingi Bilioni 22 mwaka 2024 ukilinganisha na Shilingi Bilioni 19 mwaka 2023.

Kuanzishwa kwa Benki ya Taifa ya Ushirika kutaviwezesha Vyama vya Ushirika kufanya Biashara, kupata Mikopo yenye Riba nafuu na kuviwezesha kujiendesha kibiashara na kuwalinda Wanaushirika wakiwemo Wakulima, kutokunyonywa na Taasisi za Fedha zinazotoa Mikopo yenye Riba kubwa.

1.10. Marekebisho ya Sheria ya Ushirika

Tume imefanya Marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Ushirika Na 6 ya Mwaka 2013 ambapo Marekebisho hayo yaliwalishwa katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Mkutano wake wa 18, Kikao cha Pili kwa ajili ya kusomwa kwa mara ya pili na tatu kupitia kupitia Mswada wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali, Na. 3 ya Mwaka 2024 “The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 3) Act, 2024”.

1.11. Kuimarika kwa Taswira Chanya ya Ushirika

Kutokana na Mafanikio makubwa yaliyopatikana katika Utekelezaji wa Vipaumbele vya Sekta ya Ushirika, taswira ya Ushirika imeendelea kuimarika. Mafanikio ya Ushirika yaliyopatikana na kutangazwa kwa umma ni pamoja na kuanzishwa kwa Benki ya Ushirika, kuanzishwa kwa Mfumo wa Kidigitali wa Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (MUVU), Matumizi ya Mizani za Kidigitali katika mauzo ya mazao ya wakulima, Uwazi katika Minada ya mazao ya wakulima,

Tumbaku, Korosho, Pamba, Kahawa, Ufuta, Kakao, Mkonge, Chai, Mbaazi, Soya, Dengu na Miwa. Wananchi wengi wameendelea kujiunga kwenye Vyama vya Ushirika ili kupata nguvu ya Pamoja ya soko la mazao yao na kuongeza kuimarisha Uchumi wao na Taifa kwa ujumla.



Mrajis na Mtendaji Mkuu wa TCDC, Dkt. Benson Ndiege akizungumza na waandishi wa Habari

MIKAKATI ILIYOSAIDIA KUKUA KWA SEKTA

Maendeleo ya Sekta, yanatokana na Serikali kupitia Tume ya Maendeleo ya Ushirika kufanya mambo yafuatayo:-

i. Kuongeza vitendea kazi katika Ofisi za Mikoa na Wilaya.
Tume imenunua magari **15** kwa ajili ya Ofisi za Mikoa ukilinganisha na magari 7 yaliyokuwepo Mikoani kwa mwaka 2021/22 na kufanya jumla ya mikoa **22** kuwa na magari. Aidha, Tume imenunua Kompyuta **42** kwa ajili ya kuwawezesha Maafisa Ushirika kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

ii. Mafunzo kuhusu usimamizi na uendeshaji wa Vyama vya Ushirika, yametolewa kwa Maafisa Ushirika **306** waliopo katika mikoa 20, Watendaji wa Vyama vya Ushirika **7,517,** Wanachama **40,253** na Viongozi **5,553.** Februari 2025, Manyara

iii. Tume imesimamia mchakato wa kuajiri Watendaji Wakuu wa Vyama Vikuu **44** na Miradi ya Pamoja **15.** Aidha katika kipindi hicho Tume ilfanya tathmini ya uhitaji wa watendaji katika vyama



Magari yaliyonunuliwa na TCDC katika kuimarisha Usimamizi wa Vyama vya Ushirika nchini

vikuu na miradi ya pamoja ipatayo 59 na SACCOS daraja B 142.

iv. Tume imeendelea kuimarisha matumizi ya Mfumo wa Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (MUVU) ambapo hadi kufikia Februari 2025, jumla ya vyama vya ushirika **6,634** kati ya vyama **7,820** vilivyo kwenye Daftari la Usajili wa Vyama vimesajiliwa kwenye MUVU.

v. Tume imeendelea kutekeleza Mawasiliano ya Kimkakati (Strategic Communication) katika kujenga Taswira chanya ya Ushirika. Aidha, Vyama vya Ushirika vinatekeleza kikamilifu Mwongozo wa Mawasiliano kwa Vyama ili kuongeza uelewa na manufaa ya Ushirika kwa wanachama na wananchi kwa ujumla.

WANAUSHIRIKA ZANZIBAR WAFANYA ZIARA KATIKA VYAMA VYA USHIRIKA MKOANI DODOMA



Mrajis na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Dkt. Benson Ndiege pamoja na Kaimu Mrajis Idara ya Maendeleo ya Ushirika Bi. Zainab Abdulkadiri wakisaini Randama ya Mashirikiano, Jijini Dodoma

Watumishi wa Idara ya Maendeleo ya Ushirika Zanzibar wamefanya ziara ya mafunzo katika Vyama vya Ushirika Mkoani Dodoma kwa lengo la kujifunza na kubadilishana uzoefu kuhusu Maendeleo ya Ushirika Tanzania Bara.

Katika ziara hiyo iliyofanyika tarehe 11 Machi 2025, Wanaushirika kutoka Zanzibar waliambatana na wenyeji wao Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC) na ilihusisha kutembelea vyama vya ushirika vya Akiba na Mikopo pamoja na vya Kilimo, kikiwemo K.K.K.T Arusha Road SACCOS LTD, UDOM SACCOS LTD, CHABUMA AMCOS LTD, na BBT Chinangali AMCOS LTD.

Akizungumza wakati wa ziara hiyo, Mrajisi na Mtendaji Mkuu wa TCDC, Dkt. Benson Ndiege, amesema kuwa tukio hilo limekuwa la manufaa kwa pande zote mbili, kwani limewapa fursa ya kubadilishana mawazo na kujifunza jinsi ushirika unavyofanya kazi katika Tanzania Bara na Zanzibar.

Tanzania ina Vyama vingi vya Ushirika vya aina mbalimbali, hivi tulivyotembelea leo ni sehemu ndogo tu, na nina imani kuwa mtarudi tena ili kujifunza zaidi kutoka kwa vyama vingine vilivyopo mikoa mingine," amesema Dkt. Ndiege.

Kwa upande wake, Naibu katibu Mkuu, Kazi na Uwezeshaji kutoka Ofisi ya Rais Kazi Uchumi na Uwekezaji, Halima Maulid Salum,

"amesema kuwa ziara hiyo imewapa maarifa mapya ambayo yatasaidia kuboresha Vyama vya Ushirika Zanzibar.

"Tumepata mambo mazuri sana, lakini pia tunapenda na ninyi mfike Zanzibar kuona namna tunavyotekeleza ushirika wetu. Ushirikiano wetu utaimarisha maendeleo ya sekta hii kwa pande zote mbili," alisisitiza.

Naye Mkurugenzi wa Utumishi na Uendeshaji kutoka Ofisi ya Rais – Kazi, Uchumi na Uwekezaji Zanzibar, Mohammed Jaffar, amesema kuwa vyama walivyotembelea ni mfano wa kuigwa, hasa kwa mchango wao katika kutoa ajira kwa wananchi.



Viongozi wa TCDC, Idara ya Maendeleo ya Ushirika Zanzibar pamoja na Viongozi wa KKKT Arusha Rd SACCOS katika Picha ya pamoja katika ziara ya mafunzo katika Ofisi za Chama hicho, Jijini Dodoma

"Mnafanya kazi kubwa kwa kutoa ajira za muda mfupi na za kudumu kwa wananchi, jambo ambalo linapunguza tatizo la ukosefu wa ajira nchini. Pia, mmeonesha uzalendo kwa kulipa kodi kutokana na ajira mnazozalisha na huduma mnazotoa," alisema Jaffar.

Ziara hiyo ni iliambatana na kusaini Randama ya Makubaliano (MoU) ya Ushirikiano kati ya Watumishi wa Idara ya Maendeleo ya Ushirika Zanzibar pamoja na Tume ya Maendeleo ya Ushirika





BENKI YA USHIRIKA YATAKIWA KUTUMIA FURSA ZA USHIRIKA KUJIENDESHA KIBIASHARA

Mwenyekiti wa Kamisheni ya Tume ya Maendeleo ya Ushirika (TCDC) Abdulmajid Nsekela ametoa wito kwa Benki ya Ushirika kutumia fursa za Ushirika kuongeza tija kibiashara kwa Benki hiyo.

Amesema hayo wakati Kamisheni ya Tume ilipofanya ziara ya kutembelea na kujifunza hatua za kiutendaji zilizofikiwa na Benki hiyo Machi 25, 2025 Jijini Dodoma.

Amesema ni muhimu Benki hiyo kuangalia namna bora ya kutumia Vyama vya Ushirika katika kuongeza fursa za wateja, biashara na mikopo yenye ushindani kwa Vyama.

Akieleza kuhusu Benki hiyo Mkurugenzi Mtendaji Godfrey Ng'urah amesema Benki hiyo tayari inafanya kazi na Vyama vya Ushirika kwa karibu na itaendelea kuunganisha Benki hiyo na Mifumo ya TEHAMA ili kutoa huduma kidijitali na kuwafikia wanachi wengi.

Kwa upande wake Mrajis na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Dkt. Benson Ndiege amesema Tume iko tayari kuendelea kutoa ushirikiano wakati wote ili kuhakikisha azma ya Serikali ya uanzishaji na uendeshaji wa Benki hiyo unafanyika kwa ufanisi.

Aidha, Kamisheni imetembelea Ofisi za Tume na kujadili masuala mbalimbali ya kuendeleza na kuboresha Ushirika



Mwenyekiti wa Kamisheni ya Tume ya Maendeleo ya Ushirika Abdulmajid Nsekela, Makamu Mwenyekiti Irene Madeje mara baada ya kufungua Akaunti na Benki ya Ushirika wakiwa na viongozi wa Tume, Jijini Dodoma



Kamisheni ya TCDC ikiongozwa na Mwenyekiti wa Kamisheni ya TCDC, Abdulmajid Nsekela walipofanya ziara katika Benki ya Ushirika, Jijini Dodoma

RAIS DKT. SAMIA AWATAKA WANAWAKE KUWEKEZA KATIKA MALEZI



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akihutubia wakati wa Maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani Kitaifa Mkoani Arusha

Siku ya Wanawake Duniani ni siku muhimu inayoadhimishwa kila mwaka tarehe 8 Machi ili kusherehekea mafanikio ya wanawake duniani na kuhamasisha juhudi za kupambana na changamoto zinazowakabili wanawake katika jamii.

Katika muktadha wa Tanzania, siku hii inapata umaarufu mkubwa na hufanyika kwa namna ya kipekee katika mikoa mbalimbali, Kwa mwaka huu 2025 maadhimisho hayo yamefanyika Jijini Arusha ambapo Rais wa Jamhuri ya Muuungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akifunga maadhimisho hayo Kitaifa mkoani Arusha.

Sensa ya Watu na Makazi ya Makazi ya mwaka 2022 inaonesha Tanzania ina Jumla ya Watu Millioni 61 ambao kati yao Wanawake ni Millioni 31 sawa na asilimia 51.3 na Wanaume ni Millioni 30 sawa na asilimia 48.7

Historia ya Siku ya Wanawake Duniani

Siku ya Wanawake Duniani ilianzishwa mwaka 1908, ikilenga kudai haki za kimsingi za wanawake kama vile haki ya kupiga kura, haki ya elimu, na haki ya kufanya kazi katika mazingira bora. Lengo kuu lilikuwa ni kusistiza haki ya usawa wa kijinsia na kuondoa unyanyasaji wa kijinsia katika jamii.

Jijini Arusha, Rais Dkt. Samia amewataka wanawake kuwekeza katika malezi kama kauli mbiu ilivyosisitiza “Wanawake na Wasichana 2025: Tuimarishe Haki, Usawa na Uwezeshaji”

‘’Ajenda hii maana yake ni kuwajenga sasa Watoto wetu, kizazi chetu cha kike na cha kiume, kuwapa fursa sawa. Harakati hizi zitategemea kizazi kipya cha Watoto wetu wa kike n awa kiume.Tunachokijenga, tuna kazi ya kujenga kizazi chetu chenye kuheshimiana nah ii si kazi ya sekta moja,si kazi ya Serikali peke yake,ni wazazi ni serikali, ni walimu ni jamii kwa ujumla. Kuna kazi ya kurudi kukaa kitako kulea Watoto wetu,

Hata hivyo, kwa Tanzania na miji kama Arusha, Siku ya Wanawake Duniani inahusishwa zaidi na juhudi za kuhamasisha usawa katika nyanja za kisiasa, kiuchumi, na kijamii. Arusha inashuhudia sherehe na maandamano ambayo hujumuisha wanawake kutoka katika sekta mbalimbali, pamoja na wawakilishi wa serikali na mashirika ya kiraia.

Makundi mbalimbali ya Wanawake kutoka Wizara,Taasisi, Sekta mbalimbali, mashirika ya Umma na binafsi yaliadhimisha Siku hiyo adhimu duniani, Wanawake Wanaushirika walikuwa mstari wa mbele katika maadhimisho hayo wakiwemo wanawake kutoka Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania, Benki ya Ushirika Tanzania (Coopbank) na Vyama mbalimbali vya Ushirika vya Jijini Arusha Arusha Women in Business SACCOS pamoja na ELCT ND SACCOS



Watumishi wanawake wa TCDC, wakiwa katika kongamano la wanawake kanda ya kati kuelekea kilele cha siku ya wanawake duniani, Jijini Dodoma.



Naibu Mrajis - Uhamasishaji, Consolata Kiluma, akizungumza na wanafunzi katika banda la ushirika katika maadhimisho wa siku wa wanawake duniani

Maadhimisho hayo Kitaifa yaliambatana na shughuli mbalimbali yakiwemo maonesho yaliyofanyika kwa muda wa siku nane kuanzia Machi 1, 2025 hadi Machi 8, 2025 siku ya Kilele cha maadhimisho. Wanawake katika makundi mbalimbali walionyesha shughuli zao wanazozifanya katika maeneo yao mbalimbali ya kazi hii yote ni kuonesha nafasi aliyonayo mwanamke katika jamii.

Kongamano la Wanawake Kanda ya Kati

Katika hatua nyingine Wanawake Mkoani Dodoma wameungana na Wanawake wengine wa mikoa ya Singida na Iringa kuadhimisha Siku ya Wanawake kupitia Kongamano la Wanawake wakijadili kwa kina mada ya Wanawake na Uongozi katika miaka 30ya Beijing na Kauli Mbiu ya " Wanawake na Wasichana 2025 Tuimarishe Haki, Usawa na Uwezeshaji limefanyika Machi 03,2025 Jijini Dodoma.

Mikoa mbalimbali pia iliadhimisha maadhimisho hayo kwa kushiriki kwenye majukwaa mbalimbali na kushiriki katika kutimimiza msingi wa saba wa Ushirika wa kuijali jamii,

Wanawake wanaushirika wa mkoa wa Dodoma, Arusha na Mwanza walishiriki majukwaa ya Wanawake katika mikoa yao kwa lengo la kuwaleta wanawake Pamoja na kutambua juhudi na mchango mkubwa wa Wanawake.

Siku ya Kilele huambatana na maandamano; Wanawake kutoka katika taasisi mbalimbali hufanya maandamano ya amani kuonyesha mshikamano na kuhamasisha jamii kuhusu haki za wanawake.

Aidha, Mikutano na semina ilifanyika ili kujadili changamoto zinazowakabili wanawake katika nyanja za elimu, afya, na utawala.

Shughuli mbalimbali hufanyika katika kuadhimisha siku hii ikiwemo Uzinduzi wa Miradi ya Maendeleo, utoaji wa Tuzo kwa Wanawake Bora, Elimu na Uhamasishaji pamoja na maandamano siku ya Kilele; Wanawake kutoka katika taasisi mbalimbali hufanya maandamano ya amani kuonyesha mshikamano na kuhamasisha jamii kuhusu haki za wanawake

Changamoto zinazowakabili Wanawake

Hata hivyo, licha ya mafanikio na juhudi kubwa zinazofanywa, wanawake nchini Tanzania kwa ujumla bado wanakutana na changamoto kadhaa, ikiwa ni pamoja na unyanyasaji wa Kijinsia, Ukosefu wa Fursa za Kiuchumi, Elimu na Afya:



Baadhi ya wananchi waliotembelea banda la Ushrika wakisaini katika kitabu cha wageni kwenye kilele cha siku ya wanawake yaliofanyika Jijini Arusha

Hitimisho

Siku ya Wanawake Duniani ni fursa muhimu ya kusherehekea mafanikio ya wanawake, lakini pia ni wakati wa kutathmini na kujitahidi kupambana na changamoto zinazowakabili. kama ilivyo katika nchi zingine juhudi za kuongeza usawa wa kijinsia zinaendelea, lakini bado kuna kazi kubwa ya kufanyika ili kuhakikisha kuwa wanawake wanapata haki zao zote na kuwa na fursa sawa na wanaume katika jamii. Maadhimisho haya hutoa nafasi nzuri ya kufanya hivyo, kwa kuhamasisha jamii na serikali kufanya kazi kwa pamoja kuhakikisha wanawake wanapata haki zao.





MAFUNZO YA USIMAMIZI WA VYAMA VYA USHIRIKA KWA MAAFISA USHIRIKA YANAVYOONGEZA TIJA KATIKA USHIRIKA

Kuwajengea uwezo Maafisa Ushirika ni miongoni mwa majukumu ambayo yamekuwa yakitekelezwa na Tume ya Maendeleo ya Ushirika (TCDC) kwa lengo la kuimarisha utendaji na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika.

Taarifa ya utendaji wa Sekta ya Ushirika katika Kipindi cha mwaka 2021/22 hadi 2023/24 inadhihirisha kuimarika kwa utendaji wa Vyama vya Ushirika kutokana na ongezeko la Hati safi ambapo, Hati safi zimeongezeka kutoka vyama 339 mwaka 2021/22 hadi kufikia vyama 631 Mwaka 2023/24.
Aidha, Vyama vilivyopata Hati isiyoridhisha na maoni vimepungua kutoka Vyama 1,198 mwaka 2021/22 hadi vyama 263 mwaka 2023/24 na Hati mbaya zimepungua kutoka mwaka 2023/2024. Hali hii inaashiria kuwa utendaji wa vyama vya ushirika umeimarika.

Mhe. Queen Sendiga akifungua Mafunzo ya Usimamizi wa Vyama vya Ushirika kwa Maafisa Ushirika wa Kanda ya Kaskazini mjini Babati - Manyara Februari 28, 2025 ametoa rai (TCDC) kufanya mafunzo kwa Viongozi wa Vyama vya Ushirika kama ambavyo wanapatiwa mafunzo Maafisa Ushirika.

Amesema Maafisa Ushirika waliopatiwa mafunzo wakirudi kwenye Vyama vya Ushirika wanavyovisimamia watakuwa na morali ya kubadili yale ambayo walikuwa wanayafanya bila kufuata utaratibu, ila watakosa ushirikiano kutoka kwa Viongozi wa Vyama kwasababu wao hawajapata Mafunzo hayo.

“ kumekuwa na tabia ya viongozi wa Vyama kujisahau na kuona kama vile Vyama ni mali zao binafsi na kusahau kuwa chama ni mali ya mwanachama na wanapaswa ufanye kazi kwa malengo ya Chama na si yako binafsi,” amesema Sendiga.

Ameeleza kuwa, Vyama vya Ushirika ili vifike mbali, Maadili na nidhamu ya pesa inahitajika kwa Viongozi na Maafisa Ushirika kwani vikikosekana hivyo vitu viwili hakuna Chama cha Ushirika kinaweza kupata mafanikio au kwa namna yoyote ile.

Pia ameelezea Matumizi ya TEHAMA ndiyo muelekeo wa Serikali katika kila kitu na hivyo ni muhimu Maafisa Ushirika watumie Mfumo wa MUVU katika Utendaji kazi wao hali itakayorahisisha hadi upatikanaji wa taarifa



Mkuu wa Mkoa wa Manyara Mhe. Queen Sendega akifungua Mafunzo ya Maafisa Ushirika Kanda ya Kaskazini yaliyoratibiwa na Tume, Babati Mkoani Manyara

Naye Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo anayesimamia Ushirika na Umwagiliaji, Dkt. Stephen Nindi, amesema ni matarajio ya Serikali kwamba mafunzo kwa Maafisa Ushirika yatawajengea uwezo ili kufanya kazi zao kwa umahiri na weledi ambao utaongeza ufanisi katika Vyama vya Ushirika na kupunguza kwa kiasi kikubwa kasoro mbalimbali zinazojitokeza ikiwa ni pamoja na kupunguza idadi ya Hati za ukaguzi zisizoridhisha kwa Vyama vya Ushirika.

Kwa Upande wake Mrajis na Mtendaji Mkuu Tume ya Maendeleo ya Ushirika, Dkt. Benson Ndiege, amesema Maafisa Ushirika wanaopata Mafunzo haya wanatakiwa kuzingatia na kuyafanyia kazi Mafunzo wanayopewa wakirudi katika maeneo yao ya kiutumishi.



Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo, Dkt. Stephen Nindi.

Mafunzo hayo yalijikita katika mada mbalimbali ikiwemo Maadili ya Utendaji kazi katika Utumishi wa Umma, Rushwa katika Vyama vya Ushirika, Dhana ya Ushirika, Kodi kwenye Vyama Vya Ushirika, Usimamizi wa Mikataba na nafasi ya Sheria katika ukaguzi ,Usimamizi wa Vyama vya Ushirika na Usajili, Ufuatiliaji na Ufilisi wa Vyama vya Ushirika,

Maeneo muhimu Kwenye Mfumo wa Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (MUVU) na Usimamizi wa uandaaji na utunzaji wa vitabu katika Vyama vya Ushirika, Usimamizi wa Vihatarishi kwenye Vyama vya Ushirika, Udhibiti na utatuzi wa Migogoro kwenye Vyama vya Ushirika na utunzaji wa Siri.



Mrajis na Mtendaji Mkuu Tume ya Maendeleo ya Ushirika, Dkt. Benson Ndiege.

Pia Maafisa Ushirika walipata nafasi ya kupata mafunzo ya masuala ya upimaji wa afya kwa hiari pamoja na kuchangia damu kwani Maafisa hao wamejua umuhimu wa tukio hilo baada ya kupatiwa elimu ya kupambana na VVU/UKIMWI na Magonjwa sugu yasiyoambukiza pamoja na Afya ya Akili ambayo itasaidia kutambua hali za afya zao na kuchukua hatua za kuongeza ufanisi kwenye utendaji kazi.

Ripoti ya Utafiti wa Watalii wa Kimataifa wanaoondoka nchini, 2023 iliyoandaliwa na Wizara ya maliasili na Utalii kwa kushirikiana na Benki Kuu ya Tanzania, Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) na Idara ya Uhamiaji na Kamisheni ya Utalli ya Zanzibar imebainisha Sekta ya utalii imeendelea kuimarika kutokana na ongezeko la idadi ya watalii pamoja na matumizi yao hapa nchini.

Mapato yatokanayo na utalii kwa mwaka 2023 yaliongezeka kwa asilimia 33.5 hadi kufikia dola za Marekani milioni 3,373.8 kutoka dola milioni 2,527.8 mwaka 2022. Sambamba na hilo, idadi ya wageni wa kimataifa iliongezeka kwa asilimia 24.3 hadi kufikia 1,808,205 - rekodi ya juu zaidi kuwahi kufikiwa—mwaka 2023, ikilinganishwa na watalii 1,454,920 kwa mwaka 2022.





Tume baada ya Mafunzo kwa Maafisa Ushirika iliunga mkono jitihada za Serikali ya Awamu ya Sita katika kutangaza utalii nchini kupitia 'Royal Tour' ili kukuza na kuendeleza uchumi kupitia Utalii ziara katika Hifadhi ya Taifa ya Tarangire Februari 28, 2025 baada ya Mafunzo.



Mrajis na Mtendaji Mkuu Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania, Dkt. Benson Ndiege, akifunga mafunzo hayo Machi 01, 2025 na kutoa rai kwa Maafisa Ushirika Nchini kuwa waadilifu na kuziba mianya ya rushwa katika Utendaji kazi wao.

Amesema uadilifu na maadili kazini ni jambo ambalo kila mtumishi anapaswa kulizingatia, ili kila mtumishi aweze kutekeleza wajibu wake na kuimarika katika utendaji kazi baada ya kupata mafunzo ya usimamizi wa vyama vya ushirika.

Dkt. Ndiege amesema Ushirika ni sekta ambayo inagusa wananchi moja kwa moja, hivyo Maafisa Ushirika wanapaswa kuzingatia uadilifu na kukuhakikisha wanaziba mianya ya rushwa katika utendaji kazi wao.

“Niwaambie tu rushwa ni adui wa Ushirika, zuieni mianya ya rushwa na jiepusheni na rushwa msijitie doa kwa mambo yanayoepukika,” amesema Dkt. Ndiege

Aidha, Dkt. Ndiege amesema anategemea Maafisa waliopata mafunzo wataenda kuyafanyia kazi mafunzo waliyoyapata na wataishi ndani ya hayo mafunzo ili kuboresha utendaji kazi wao wa kila siku.

Kwa upande wake Mwakilishi wa Maafisa Ushirika, Sofia Shoko, ametoa shukrani kwa Tume ya Maendeleo ya Ushirika kuwapatia mafunzo ambayo yamewayamewajenga na kuwaongezea ufanisi na weledi katika utendaji kazi wa kila siku.



Naibu Mrajis - Udhibiti, Collins Nyakunga

AFRIKA INAHITAJI KUREJESHA HADHI YAKE KWENYE TASNIA YA KAHAWA DUNIANI - RAIS DKT. SAMIA



Rais wa Jamhuri ya muungano wa Tanzania, Mh. Dkt. Samia Suluhu Hassan, akipokea maelezo kutoka kwa Waziri wa Kilimo Mh. Hussein Bashe katika Mkutano wa Tatu wa nchi 25 wazalishaji wa Kahawa Barani Afrika

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, amesema Afrika inahitaji kurejesha hadhi yake kwenye tasnia ya Kahawa Duniani.

Mhe. Rais Dkt. Samia amepongeza nchi za Afrika kuja pamoja kujadili uendelezaji wa zao hilo na Umoja wa Afrika kuliingizia zao la Kahawa kwenye mazao ya kimkakati hatua ambazo ni muhimu katika kuanza kurejesha hadhi ya Afika kwenye tasnia ya Kahawa duniani.

Rais Dkt. Samia ameyasema hayo leo Februari 22, 2025 katika Mkutano wa Tatu wa nchi 25 wazalishaji wa Kahawa Barani Afrika uliofanyika katika ukumbi wa Mikutano wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNICC) Jijini Dar es salaam.

Rais Dkt. Samia amesema, licha ya tasnia ya Kahawa kukabiliwa na changamoto anuai, amoto anuai, Bara la Afrika limeanza kupiga hatua katika kukabiliana na changamoto hizo

Aidha, ameeleza imani yake ya kuwa na jukwaa hilo la nchi wazalishaji wa Kahawa Barani Afrika litaweza kuunganisha nguvu katika kukabiliana na changamoto zinazoikumba Sekta ya Kahawa Barani Afrika na kuwa nyenzo sahihi ya kufikia malengo waliyojiwekea.
Kwa upande mwingine, Rais Dkt. Samia amezitaka nchi za Afrika ziazimie kuwa ifikapo 2035 nusu ya Kahawa inayozalishwa Barani Afrika iongezewe thamani Barani Afrika kabla ya kuuzwa ndani na nje ya bara hilo.
Akifafanua kuhusu manufaa ya zao la kahawa, Rais Dkt. Samia amesema takwimu zinaonesha kuwa manufaa zaidi ya zao hilo yapo kwenye mnyororo wa thamani mzima kuliko uzalishaji. Hivyo, Afrika inahitaji kuwa na viwanda vingi zaidi vya kuchakata Kahawa na vya kutengeneza bidhaa nyingine zinazotokana na mabaki ya zao hili.

Rais Dkt. Samia amesema kuendelea kusafirisha Kahawa ghafi ni kuendelea kusafirisha ajira za vijana zinazohitajika Afrika, kujikosesha mapato zaidi ambayo yanahitajika kwa maendeleo ya Bara la Afrika na kumfanya mkulima wa Kahawa aendelee kukosa soko la uhakika wa anachokizalisha.



Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko, katika mkutano kuhusu masuala ya mazao jamii ya mikundeuliofanyika Nchini India.

SERIKALI YAJIDHATITI KUBORESHA SEKTA YA KILIMO – DKT BITEKO

Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko, amesema Serikali ya Tanzania imejidhatiti kuboresha na kuimarisha Sekta ya Kilimo kwa kuja na mipango kadhaa yenye lengo la kuongeza fursa kwa wakulima nchini.

Dkt. Biteko amesema hayo jijini New Delhi, India wakati akishiriki mkutano kuhusu masuala ya mazao jamii ya mikunde.
"Tunaongeza uwekezaji katika utafiti na kuboresha upatikanaji wa teknolojia za kisasa za kilimo ambapo kila afisa wa ugani nchini amepewa vifaa vyote muhimu ikiwemo pikipiki na kompyuta ili kutoa huduma nzuri na kwa wakati kwa wakulima wetu." Amesema Dkt. Biteko

Amesema Serikali pia imeboresha shughuli za usafirishaji wa bidhaa ikiwa ni pamoja na kurahisisha michakato ya uuzaji mazao, "Tanzania inaendeleza ujenzi wa reli ya kisasa (SGR) ambayo itaimarisha usafirishaji wa bidhaa yenye urefu wa takribkilomita 500 kutoka Bandari ya Dar es Salaam hadi Dodoma ambayo imekamilika na na inatumika.

Vilevile, amesema kupitia mradi wa BBT (Building a Better Tomorrow) Serikali imewezesha vijana kwa kuwapa ardhi, fedha na upatikanaji wa masoko sambamba na kuongeza huduma za kifedha za kidijitali.

Aidha, Dkt. Biteko amesema "India ni soko muhimu kwa mazao jamii ya kunde kutoka Tanzania na tunaweza kupata mafanikio makubwa zaidi. Leo nawaalika wawekezaji kutoka India na nchi nyingine duniani kuja kuwekeza katika sekta ya kilimo ya Tanzania kuanzia uzalishaji wa kisasa wa soya hadi uwekezaji katika mifumo ya usimamizi wa mavuno,"

Akizungumzia maendeleo ya sekta mazao jamii ya mikunde, amesema kuwa mwaka 2023, Tanzania ilizalisha takriban tani 250,000 za mbaazi, ikiwa ni ongezeko la asilia amesema kuwa mwaka 2023, Tanzania ilizalisha takriban tani 250,000 za mbaazi, ikiwa ni ongezeko la asilimia 56 ikilinganishwa na mwaka 2018.

Inakadiriwa ifikapo mwaka 2030 Tanzania itakuwa na ukuaji mkubwa katika Pato la Taifa kupitia Kilimo, ambapo mauzo ya maharage mekundu, mbaazi na choroko yanatarajiwa kufikia dola bilioni 1.47, dola milioni 84 na dola milioni 115. Aidha, ili kufikia uwezo huo, Tanzania imeweka mikakati ya kukuza sekta ya mazao jamii ya kunde kupitia Mfumo wa Stakabadhi Ghalani kwa wakulima kusajiliwa, kuboresha mbinu za kilimo na teknolojia, kuhakikisha ubora na viwango vya mazao kulingana na mahitaji ya soko.

Pamoja na hayo Dkt. Biteko amesema "Mazao jamii ya kunde nchini Tanzania yanauzwa kupitia mnada wa mtandaoni ambao unatoa fursa kwa wafanyabiashara kupata taarifa kuhusu mizigo iliyohifadhiwa katika ghala lililosajiliwa,"

Amesisitiza “Mfumo huu unahakikisha uwazi, ufuatiliaji na ufanisi katika biashara ya kimataifa. Mwaka 2024 pekee kupitia mfumo huu, wakulima wa Tanzania walipata zaidi ya dola milioni 91.31 kutoka katika biashara ya mbaazi, dengu na maharagwe ya soya, ubunifu huu si tu unaimarisha ushindani wetu bali pia unafungua fursa mpya za ushirikiano,”

Kufuatia hali hiyo,kiwango cha biashara kati ya nchi hizo mbili kimeongezeka na kufikia dola bilioni 7.9 kwa mwaka wa fedha 2023/2024. Pia, mwaka 2023 mauzo ya mbaazi kutoka Tanzania kwenda India yalifikia tani 186,447 yenye thamani ya dola milioni 139.1.
(Na Ofisi ya Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati).



CHAMA KIKUU CHA USHIRIKA NYANZA CHAZINDUA UVUNAJI WA SAMAKI WA VIZIMBA

Chama Kikuu cha Ushirika Nyanza (NCU LTD) kimezindua uvunaji wa samaki wa vizimba katika ziwa Victoria Jijini Mwanza.

Uzinduzi huo umefanyika tarehe 10 Februari 2025 na umeshuhudiwa na Mrajis Msaidizi wa Vyama vya Ushirika Mkoa wa Mwanza, Hilda Boniface, kutokana na chama kupata wateja wengi wa samaki.

"Serikali tunaunga mkono juhudi hizi zinazofanywa na NCU LTD za kuhakikisha wamesimamia vyema mradi huu na kuweza kufikia hatua ya uvunaji ambapo hii ni sehemu ya chanzo kimojawapo cha mapato kwa chama," amesema Hilda.





Mrajis Msaidizi ameitaka NCU LTD kukuza na kupanua mradi kwa maslahi mapana ya wanachama wake pamoja na kuzidi kujiimarisha kwa kufanya Ushirika kibishara ili kutengeneza faida kubwa.

JE WAJUA, TAARIFA ZINAZOPASWA KUWA KATIKA REJESTA YA CHAMA CHA USHIRIKA?

Kila chama cha ushirika kitapaswa kuwa na kutunza Rejista ya wanachama na kuhakikisha kwamba Rejista itakuwa na:

(a) Jina na anwani ya mwanachama;

(b) Namba ya usajili ya mwanachama;

(c) Idadi na thamani ya hisa zilizolipiwa;

(d) Pale inapohitajika, jina na anwani ya mrithi;


(e) Tarehe ya uthibitisho;

(f) Tarehe ya usajili wa uanachama

(g) Tamko la kufuata masharti ya chama; na

(h) Taarifa nyingine kama ilivyo katika masharti ya chama.

UNION NA SACCOS KUBWA ZATAKIWA KUAJIRI WAKAGUZI WA NDANI







Mrajis wa vyama vya Ushirika, Dkt. Benson Ndiege, katika picha ya pamoja na kamati ya ukaguzi ya TCDC wakati wa uzinduzi wa kamati hiyo, Jijini Dodoma.

Mrajis na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC), Dkt. Benson Ndiege ameagiza Vyama Vikuu vya Ushirika na SACCOS kubwa nchini kuajiri na kuwatumia ipasavyo Wakaguzi wa Ndani ili kuongeza ufanisi wa vyama hivyo.

Dkt. Ndiege ameyasema hayo leo Januari 14, 2025 Jijini Dodoma wakati akizindua Kamati ya Ukaguzi ya TCDC ambapo amesema Wakaguzi ni watendaji muhimu wanaohitajika kusaidia kubaini changamoto za kwenye ushirika na kushauri namna ya kukabiliana nazo ili kuendelea kuwa na usimamizi imara wa Sekta ya Ushirika.

“Serikali imedhamiria kuimarisha ushirika kwa maslahi mapana ya nchi, Tume hii ni chombo muhimu na kinaangaliwa kwa jicho la pekee kwa maslahi makubwa ya nchi yetu, hivi sasa tuna takribani vyama vya ushirika 7,000 na vilivyosajiliwa kwenye Mfumo wa kielektroniki wa Usimamizi wa Vyama vya Ushirika ni 6,500 baadae tutatoa takwimu kama vipo ambavyo havifanyi kazi,”amesema.

Aidha, amesema serikali ya awamu ya sita imeipa uzito sekta ya ushirika na kwamba Tume hiyo ni chombo muhimu kwa serikali na mfumo pekee utakaowasaidia watanzania ni ushirika ili kuwa na nguvu ya pamoja ambapo takriban watu milioni nane wanajihusisha na vyama vya ushirika.

Dkt.Ndiege amesema ni lazima Tume ambayo ni msimamizi wa sekta ya ushirika kuwa imara na wajumbe wa kamati hiyo walioteuliwa wameingia kwa sifa na uwezo wao wa kufanya kazi ili kusaidia usimamizi wa Vyama vya Ushirika.

Awali, Mwenyekiti Mstaafu wa Kamati hiyo, CPA Evance Assenga amesema kamati yake ilishauri na kuhakikisha kunakuwa na matumizi sahihi ya rasilimali, uwazi na uwajibikaji wa Tume ili kuleta ufanisi kwenye sekta hiyo, huku akiishauri kamati mpya kutumia kutumia kwa umakini taarifa za Mkaguzi wa Ndani kwa kuwa zitawasaidia kwenye ukaguzi.

Naye, Mwenyekiti wa Mpya wa kamati hiyo, CPA Elihuruma Lema ameahidi kufanya kazi hiyo kwa ufanisi na weledi mkubwa ili kuongeza tija kwenye sekta ya ushirika nchini ambayo ina idadi kubwa ya watu wanaochangia uchumi wa nchi

TENGENEZENI MIFUMO,TARATIBU NA KANUNI IMARA ILI KUENDELEZA VYAMA - NAIBU KATIBU MKUU KILIMO



Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo, Dkt. Stephen Nindi (Katikati), Mrajis na Mtendaji Mkuu wa TCDC, Dkt. Benson Ndiege, (kulia), Makamu mwanyekiti wa kamisheni ya Ushirika, Irene Madeje na viongozi wengine katika picha ya pamoja baada ya kikao kazi cha TCDC, TFC na SCCULT

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo anayesimamia Ushirika na Umwagiliaji, Dkt. Stephen Nindi amezitaka Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC), Shirikisho la Vyama vya Ushirika (TFC) na Muungano wa Vyama vya Ushirika (SCCULT) kuhakikisha kuwa wanatengeneza Mifumo, Taratibu na Kanuni imara ili kuendeleza Vyama Ushirika vilivyo imara.

Ametoa rai hiyo leo Januari 10, 2025 katika kikao kazi cha kujadili mwelekeo wa Serikali kuhusu Maendeleo ya Ushirika nchini kilichowashirikisha Tume ya Maendeleo ya Ushirika (TCDC), Shirikisho la Vyama vya Ushirika (TFC) na Muungano wa Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo (SCCULT) kilichofanyika Jijini Dodoma.

"Serikali inatambua jitihada zinazofanywa na Tume ya Maendeleo ya Ushirika katika kuhakikisha inasimamia vyema Vyama vya Ushirika ila jambo la muhimu serikali inalolitaka kwenu TCDC, TFC na SCCULT, tengenezeni Mifumo, taratibu na Kanuni imara ili kuendeleza Vyama na kuwa na Ushirika imara na wenye nguvu," amesema Dkt. Nindi.

Aidha, ameongeza kuwa hakuna haja ya kuwa na utitiri wa Vyama vya Ushirika ambavyo havisaidii katika kukuza Sekta ya Ushirika ni bora kuwa na Vyama vichache ambavyo vitasimama imara na kuweza kuwatetea Wanachama hasa Wakulima ambao ndio wazalishaji wakubwa wa mazao ya kibiashara na hivyo kuimarisha Sekta ya Kilimo hapa nchini.

Naye Makamu Mwenyekiti wa Kamisheni ya Ushirika, Irene Madeje, amesema kuwa ili kujenga taswira ya Ushirika iliyosimama kibiashara na Ushirika imara na wenye nguvu ni lazima Vyama vizingatie maelekezo ya Serikali na kutekeleza Vipaumbele vinane vya Ushirika vilivyotolewa na Kamisheni na Wanaushirika.

Akivitaja vipaumbele hivyo kuwa ni, Uwekezaji katika Mifumo ya kisasa ya kidigitali, Kuimarisha Maendeleo ya Benki ya Ushirika, Kuhamsisha Mfumo wa Ushirika kujiendesha kibiashara, Kuboresha Sera, Sheria na Usimamizi wa Ushirika, Kuhamasisha Ushirika kwenye Sekta mbalimbali na Makundi maalumu, Kuimarisha Uwekezaji na Mali za Ushirika katika uzalishaji, kushirikiana na Wadau mbalimbali katika kutatua changamoto zilizopo kwenye

Watumishi na Mazingira ya Utendaji kazi.

Kwa upande wake, Mrajis na Mtendaji Mkuu wa TCDC, Dkt. Benson Ndiege, ametoa rai kwa Bodi za TFC na SCCULT kuhakikisha kuwa Ushirika unamnufaisha kwanza Mwanaushirika mwenyewe na si vinginevyo na kusisitiza Ushirikiano baina ya TCDC na Bodi hizi ili kuweza kutoka hatua moja na kwenda hatua nyingine katika kuendeleza Vyama vya Ushirika.

"Nitoe wito kwenu TFC, SCCULT na Vyama vya Ushirika kuhakikisha mnashirikiana Vema na TCDC ili kuhakikisha yale mazuri tunayoyafanya katika katika Vyama vyetu yanatangazwa na hivyo kuleta mwamko na kuhamasisha Wananchi wengi zaidi wanafahamu mazuri ya Sekta ya Ushirika na si vinginevyo," ameyasema Dkt. Ndiege.



Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo, Dkt. Stephen Nindi, akitoa maelekezo kwa viongozi wa bodi za TCDC, TFC na SCCULT

TCDC NA WAKANDI ZASAINI 'MoU' KUVIIMARISHA VYAMA VYA USHIRIKA KIDIGITALI



Mtendaji Mkuu wa TCDC, Dkt. Benson Ndiege, (kulia) akisaini Randama ya Makubalino (MoU) na Shirika la WAKANDI

Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC) na Shirika la WAKANDI Tanzania LTD wamesaini Randama ya Makubalino (MoU) ili kuviwezesha Vyama vya Ushirika nchini kujiimarisha katika matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA).

Makubalino hayo yametiwa saini Jijini Dar es Salaam leo Machi 7, 2025 na Mrajis na Mtendaji Mkuu wa TCDC, Dkt. Benson Ndiege na Mwenyekiti wa WAKANDI Tanzania LTD, Richard Sinamtwa.

Shirika la WAKANDI ni taasisi isiyokuwa ya kiserikali inayotoa usaidizi wa kifedha na Mifumo ya TEHAMA kwa Vyama vya Ushirika na Taasisi za kifedha Afrika kwa ufadhili wa nchi ya Norway.

Akizungumza katika hafla hiyo Mrajis wa Vyama vya Ushirika na Mtendaji Mkuu wa TCDC, Dkt. Benson Ndiege, ameitaka WAKANDI na Vyama vya Ushirika vitakavyopata usaidizi kufuata Sheria na taratibu za nchi wakati wa utekelezaji wa Mpango huo ili kuviwezesha Vyama kujiendesha kibiashara.

Aidha, Mtendaji Mkuu wa WAKANDI, Espen Kvelland, amesema Shirika lake litatoa huduma zilizoanishwa katika randama ya Makubalino kwa weledi na kufuata Sheria na taratibu za nchi ili kuwapatia Wanaushirika usaidizi unaohitajika kuviwezesha Vyama kujiendesha kwa faida.

Mwenyekiti wa WAKANDI Tanzania LTD, Richard Sinamtwa amesema WAKANDI itashirikiana na TCDC amesema WAKANDI itashirikiana na TCDC katika kuendeleza Vyama vya Ushirika Kidigitali ili kuwawezesha Wanaushirika kuwa na nguvu ya pamoja kiuchumi kupitia Mifumo ya TEHAMA.

Balozi wa Norway nchini, Mhe. Tonne Tinnes, amesema nchi yake imekuwa tayari wakati wote kusaidiana na Serikali ya Tanzania kuwaletea Wananchi wake maendeleo kupitia miradi mbalimbali inayotekelezwa kwa ufadhili wa Norway.

Nchi nyingine 30 za Afrika zinafanya kazi kwa ushirikiano na WAKANDI ikiwemo Afrika ya Kusini, Kenya na Uganda ambao wamehudhuria hafla ya kusaini Makubalino kati ya TCDC na WAKANDI.

NANYUMBU AMCOS YANUNUA GARI LENYE THAMANI YA SHILINGI MIL.185



Naibu Mrajis - Udhibiti, Collins Nyakunga (katikati), Mrajis wa mkoa wa Mtwara Grace Msambaji na viongozi na wanachama katika picha ya pamoja baada ya kuzindua gari la chama hicho

Chama cha Ushirika cha msingi Nanyumbu AMCOS LTD kilichopo wilayani Nanyumbu mkoani Mtwara kimenunua gari lenye thaman ya Shilingi millioni 185, zilizotokana na bei nzuri ya mazao ya korosho kwa msimu uliopita 2024/2025.



Akisoma taarifa katika makabidhiano ya gari hilo, Katibu wa Nanyumbu AMCOS, Bakari Nakanga alisema AMCOS yao yenye wanachama 468 waliamua kununua gari hilo kwa mkopo kutoka benki ya CRDB tawi la Nanyumbu. Meneja wa benki hiyo tawi la Nanyumbu, James Kisumo amethibitisha kuwapatia mkopo huo Nanyumbu AMCOS ili waweze kurahisisha ukusanyaji wa mazao kama korosho na ufuta.

Makabidhiano ya gari hilo yalihudhuriwa na viongozi mbalimbali akiwemo Naibu Mrajis wa Vyama vya Ushirika (Udhibiti), Collins Nyakunga, ambaye alikipongeza Chama hicho kwa ushirikiao wao na kwa kuamua kununua gari hilo.

Aidha, Naibu Mrajis Nyakunga amempongeza Mrajis Msaidizi wa Vyama vya Ushirika mkoa wa Mtwara, Grace Masambaji kwa kusimamia ipasavyo vyama vya Ushirika pamoja na kutatua migogoro pale inapotokea.

Mwenyekiti wa Chama Kikuu Cha Ushirika kinachohudumia Mtwara, Nanyamba, Masasi na Nanyumbu (MAMCU), Alhaji Azam Mfaume, aliwapongeza Wana Nanyumbu AMCOS kwa maamuzi ya kununua gari kwani litawasaidia katika ukusanyaji wa mazao kupeleka ghala kuu; na amewaaasa kulitunza gari hilo ili liwapatie kipato zaidi.

Hafla hiyo ilihudhuriwa pia na Mkuu wa wilaya ya Nanyumbu, Mhe. Christopher Magala mbinu na miradi mbalimbali ili ambaye alikabidhi gari hilo, na kuwaasa viongozi wa Nanyumbu AMCOS kuendelea kubuni mbinu na miradi mbalimbali ili wazidi kupiga hatua kiuchumi.

KWA HABARI, MATUKIO NA TAARIFA KUHUSU USHIRIKA TEMBELEA MITANDAO YETU YA KIJAMII

ushirika_tcdc

Tume ya Maendeleo ya Ushirika

www.ushirika.go.tz

Ushirika Tv



Limetolewa na
Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC)
Mtaa wa Kuu, S. L. P. 201, DODOMA
Simu: +255262322456, Telefax: +255262321973
Barua Pepe: ushirika@ushirika.go.tz Tovuti: www.ushirika.